

CHUO CHA USIMAMIZI WA FEDHA



YAH: TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ADA YA MAOMBI YA UDAHILI

Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kinapenda kuwataarifu watu wote wanaotarajia na waliokwisha kufanya maombi ya udahili ili kujiunga na chuo kwa mwaka wa masomo 2017/2018 kwamba, ada ya kuomba udahili kwa kozi zote ni Tsh. 10,000/= kuanzia leo tarehe 27/7/2017. Aidha tunapenda kuwataarifu kwamba, yeyote aliyepomba nafasi ya kujiunga na chuo na kulipa gharama ya awali ya udahili atunze kumbukumbu yake ya malipo. Iwapo atachaguliwa, fedha iliyozidi itakuwa sehemu ya ada, kwa yule ambaye hatochaguliwa atarudishiwa kiasi kinachobaki kwa utaratibu utakaowekwa na chuo.

Chuo cha Usimamizi wa Fedha kinawakaribisha sana kujiunga katika kozi mbalimbali zinazotolewa na chuo hiki. Tunazidi kuwashukuru kwa kuchagua chuo hiki kuwa sehemu ya kupata elimu ya juu. .

Tunatanguliza shukrani.

Imetolewa na Ofisi ya Uhusiano

Tarehe 27/7/2017.